# EE YESU NIHURUMIE

Marcus Ab' Mtinga
15.07.2000: Musoma

**Taratibu**










**Copied By: G. M .Kombo - Capella Software**

2. Ee Bwana ninakiri udhaifu wangu wo-te, Unaujua wazi sidiriki kudanga-nya,
Na sasa naona haya kwa dhambi nyingi nilizo nazo, nachoka kuishi ji-nsi nilivyo ninaona uchungu.
Unihurumie, unisamehe Bwana ninaumia, ninasikitika ho-fu ni kubwa mwili hauna nguvu.

3. Popote nipitapo watu hunisema sa-na, Ni wengi hunifyonya hutikisa vichwa vya-o,
Ni maisha gani haya tazama Bwana yanavyotisha, sina mbele wala nyu-ma mi-mi kweli ninashangaza.
Tamaa za mwili ona zinavyoiangamiza roho, adhabu inayoku-ja hakika ni ngumu kuitaja.

4. Ee Yesu ulikufa kwa ajili yangu mi-mi, Lakini ona sasa nilivyochanganyiki-wa,
Si m--tu si mnyama ninasi-kitisha sana, wanyama ndege sama-ki wadudu nao wanashangaa.
Wanataka kunitenga sijui sasa niende wapi, Ee Yesu nihurumi-e nisaidie mwokozi wangu.

5. Ee Yesu ndiwe nguvu kwa wanyonge na dhai-fu, Naomba unigeuze niwe mtu mnyo-fu,
Niuvue mwili mwovu na kwa hasira utupwe mbali, ni maisha gani ha-ya taabu nyingi huzuni tele.
Niwavute watu wengi wakufuate mwokozi wangu, na mwisho nifike kwa-ko kwenye furaha uzima tele.